


# SHERIA NA HAKI

*Kwa kila Mwananchi*



Iwe shauku

Toleo Na. 009

Jarida la kila miezi mitatu

Januari - Machi, 2012

## Rais wa Zanzibar Aipongeze ZLSC

**R**AIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein amekipongeza Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa elimu ya sheria kwa jamii.

Dk. Shein alitoa pongezi hizo alipokuwa akitoa hotuba yake katika

sherehe za kwanza za kihistoria za kuadhimisha Siku ya Sheria Zanzibar (Zanzibar Law Day) zilizofanyika katika viwanja vya Victoria Gardens, Mji Mkongwe, Zanzibar, Februari 7, mwaka huu.

Rais wa Zanzibar alisema

anafurahishwa na vipindi vya sheria vinavyoendeshwa na ZLSC na kuonyeshwa katika Televiseni Zanzibar iliyo chini ya Shirika la Utangazaji Zanzibar.

*"Nimejenga tabia ya kutizama vipindi vya sheria vinavyoendeshwa na Kituo. Inaendelea Uk. 3*

### YALIYOMO

Buriani Mwanasheria Mkongwe  
Dourado Uk. 2

Jarida Sheria na Haki latimiza  
miaka miwili Uk. 3

Msaidizi wa Sheria afariki Uk. 4

Haki za Mshtakiwa/Mtuhumiwa  
Mahkamani Uk. 12

Wananchi Washiriki Mchakato wa  
Katiba Mpya Uk. 14

Bunge Maalum la Katiba  
(Constituent Assembly) Uk. 17



Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein akihutubia katika sherehe za Siku ya Sheria Zanzibar katika viwanja vya Victoria Gardens, Zanzibar, Februari 7, 2011.

## ZLSC Yapata 'Paralegals' Wapya

**K**ITUO cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kimepata Wasaidizi wa Sheria (paralegals) wapya 65 walioanza kazi mwezi wa Januari, 2012.

Afisa Mipango Dhamana wa Wasaidizi wa Sheria, Mtumwa Said Sandai, alisema kwamba Wasaidizi wa Sheria 37 wanatoka Unguja na 28 wanatoka Pemba.

Alisema Wasaidizi wa Sheria wamechaguliwa kutoka kila jimbo la uchaguzi Unguja na Pemba na baadhi


Inaendelea Uk. 3



Baadhi ya Wasaidizi wa Sheria wapya wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) wakisikiliza mafunzo ya awali ya Sheria kutoka kwa Mwalimu Ali Uki katika ukumbi wa EACROTANAL mjini Zanzibar.

# SHERIA NA HAKI

Kwa kila Mwananchi



Iwe shauku

Toleo Na. 009

Jarida la kila miezi mitatu

Januari - Machi, 2012

## Zanzibar Yasherehekea Siku ya Sheria kwa Mbwembwe

**Z**ANZIBAR imeandika ukurasa mpya wa historia kwa kusherehekea Siku ya Sheria (Law Day) Februari 07, 2012, kwa mara ya kwanza. Siku hii itasherehekiwa kila mwaka.

Sherehe za Siku ya Sheria zilifanyika katika viwanja vya Victoria Garden na kuhudhuriwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein,


wageni kutoka Tanzania Bara na viongozi mbali mbali wa Serikali, mawakili na wanasheria.

Sherehe hizo zilipambwa kwa mbwembwe mbali mbali pamoja na majaji, mahakimu na mawakili waliovalia nguo zao rasmi za Mahkama na kutayarisha gwaride kutoka viwanja vya Victoria Garden mpaka katika jengo la Mahkama Kuu Zanzibar. Gwaride hilo liliongozwa na

Bendi ya Polisi.

Madhumuni makubwa ya kusherehekea Siku ya Sheria ni kutoa nafasi kwa Mahkama na wadau wake wa sheria kutathmini utendeji kazi na changamoto kwa mwaka uliopita. Kauli mbiu ya mwaka huu wa sherehe za Siku ya Sheria ni "Piga Vita Rushwa katika Utendaji Haki".

Inaendelea Uk. 19



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein katika picha ya pamoja na Majaji wa Mahkama Kuu Zanzibar na baadhi ya viongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika Siku ya Sheria Zanzibar.

## Jaji Dourado Afariki Dunia


**A**LIYEKUWA Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Wolfango Joseph Dourado (83) amefariki dunia Zanzibar Machi 19, 2012 na amezikwa Machi 20, 2012 katika makaburi ya Mwanakwerekwe, nje kidogo ya Manispaa ya Zanzibar.

Marehemu Dourado alifariki katika Hospitali binafsi, baada ya kupeleka akisumbuliwa na shinikizo la damu.

Ibada ya mwisho ya kumuwaga marehemu Dourado ilifanyika katika Kanisa la Roman la Minara Miwili liliopo katika Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Mamia ya wakaazi wa Zanzibar walioongozwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti

Inaendelea Uk. 19



Marehemu Jaji Dourado